JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

DESEMBA 18, 2020

MILIONI 79.7 ZIKIWEMO KODI ZA SERIKALI (SERVICE LEVY) NA FEDHA MBALIMBALI ZA WANANCHI, ZAOKOLEWA NA TAKUKURU ARUMERU

Ndg . Wanahabari,

Leo ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Arusha imeawaita ili kuuhabarisha umma juu ya matukio makuu mawili ambayo tutayafanya leo. Tukio la kwanza litahusu kukabidhi fedha zilizookolewa na ofisi ya TAKUKURU Arumeru kwa kipindi cha Mwezi Desemba 2020. Tukio la pili ni kutangaza mkakati maalum wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha wa kushughulikia kero ya rushwa kwa kushirikiana na wananchi.

Ndg . Wanahabari,

Katika tukio la kwanza tunapenda kuufahamisha umma kwamba, katika kipindi cha mwezi Desemba 2020, ofisi ya TAKUKURU wilaya ya Arumeru imeokoa fedha kiasi cha Shilingi Milioni Sabini na Tisa, Laki Saba Themanini na Tatu elfu, Mia Moja na Themanini na Nne (**Sh. 79,783,184/=).** Fedha

hizo zilizookolewa zitakabidhiwa kwa wahusika wakiwemo watendaji wa serikali hapa mbele yenu na Mh. Jerry Muro ambaye ni Mkuu wa wilaya ya Arumeru ili ziweze kuingizwa serikalini.Fedha hizo ni za kodi ya ushuru wa huduma(Service Levy),Tozo za vibali vya ujenzi, Vyama vya ushirika, NSSF na za wananchi wanyonge ambao walitaka kudhulumiwa fedha zao kwa nyakati tofauti tofauti.Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa hapa chini.

Ndg. Wanahabari,

1. **Services Levy na Vibali vya ujenzi**

Kama ambavyo inafahamika, ukusanyaji wa tozo na kodi mbalimbali katika Halmashauri zetu ni moja ya vipaumbele muhimu vya serikali, lakini kumekuwepo na baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi na tozo hizo kwa kula njama na kushirikiana na baadhi ya watumishi wachache wasio waadilifu ambao wanahujumu kodi na tozo hizo kwa maslahi yao binafsi. Vitendo hivi huisababishia serikali hasara kwa kukosa mapato yake na kuhujumu uchumi wa nchi yetu.

TAKUKURU Arumeru imefuatilia ukiukwaji wa taratibu katika ukusanyaji wa ushuru wa huduma (SERVICE LEVY) pamoja na vibali hewa vya ujenzi vilivyotolewa na kubaini upotevu wa kiasi cha Shilingi Milioni Ishirini na Saba, Laki Tatu na Ishirini na Saba Elfu,Mia Nane Themanini na Nne (**Sh. 27,327,884/=)** ambacho kimeokolewa na fedha hizo zitakabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru kwa ajili ya kutumika kwa mujibu wa bajeti ya halmashauri.

Ndg . Wanahabari,

2. **Fedha za NSSF,Vyama vya Ushirika na Wananchi**

Fedha zingine kiasi cha Shilingi Milioni Hamsini na Mbili, Laki Nne Hamsini Tano Elfu na Mia Tatu (**Sh. 52,455,300/=)** zitakabidhiwa NSSF, Vyama vya Ushirika na kwa wananchi mbalimbali wa wilaya ya Arumeru ambao walidhulumiwa fedha zao aidha na wananchi wenzao au taasisi zilizokuwa zimewaajiri.

Ndg. Wanahabari,

Naomba kutoa wito kwa wananchi wote wakiwemo watumishi wa Serikali kuhakikisha kuwa wanafuata Sheria, Kanuni, Taratibu zinazoongoza utekelezaji wa Majukumu ya Serikali na kutambua kwamba yeyote atakayebainika kwenda kinyume, rungu la TAKUKURU litamfikia popote alipo.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inapenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa jamii kuipa ushirikiano kwa kutoa taarifa zinazohusiana na vitendo vya rushwa. Aidha, inawataka wananchi kujiepusha na vitendo vyote vya rushwa, utapeli, ulaghai, hila na dhuluma.

Ndg. Wanahabari,

Katika Tukio la pili, TAKUKURU Mkoa wa Arusha inapenda kuufahamisha umma kwamba imetenga **Siku Maalum** ya kupokea na kusikiliza malalamiko mbalimbali ya wananchi yanayohusu vitendo vya rushwa.

Ndugu waandishi wa habari, wananchi mliopo hapa na wananchi wote wa mkoa wa Arusha, jukumu la msingi la TAKUKURU ni kuratibu na kuongoza mapambano dhidi ya rushwa. Hii inamaanisha kwamba mapambano dhidi ya rushwa si ya TAKUKURU peke yake bali ni ya kila mmoja wetu (kila mwananchi). Hivyo ili kufikia malengo ya mapambano dhidi ya rushwa nchini, kila mwananchi anawajibu wa kushiriki kwa namna moja au

nyingine. TAKUKURU inamwaasa kila mwananchi kushiriki mapambano dhidi ya rushwa, kwasababu madhara ya rushwa yanamgusa kila mmoja kwa namna moja au nyingine. Kwa lugha rahisi, hakuna mtu mwenye kinga dhidi ya madhara yatokanayo na vitendo vya rushwa.

Kwa kutambua umuhimu wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa na kwa nia dhabiti ya TAKUKURU kuhakikisha kuwa vita dhidi ya rushwa inafanikiwa, TAKUKURU Mkoa wa Arusha imetenga siku ya **Jumatano ya mwisho ya kila mwezi, saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana** kuwa siku ya kupokea na kusikiliza malalamiko ya vitendo vya rushwa. Siku hii ni kwa ofisi zote za TAKUKURU Mkoa wa Arusha (Arusha, Arumeru, Monduli ,Longido, Karatu na Ngorongoro). Wananchi wanakaribishwa kufika katika ofisi yoyote ya TAKUKURU katika wilaya waliopo mkoani Arusha na kutoa malalamiko yao.

Natumia nafasi hii kuviomba vyombo vya habari na wananchi wote wanaonisikiliza, kufikisha ujumbe huu kwa wananchi wengine wa mkoa wa Arusha ili waitumie siku hii maalum kuwasilisha malalamiko yao TAKUKURU na tunawahakikishia malalamiko ypte yatakayopokelewa yatafanyiwa kazi kwa wakati na kupewa mrejesho. Toa taarifa ya vitendo vya rushwa kwa kufika ofisi ya TAKUKURU iliyopo karibu nawe au piga simu kwa namba ya bure 113 taarifa yako itapokelewa na kufanyiwa kazi.

Aidha,natumia fursa hii kuwaomba wananchi kuendelea kuiamini TAKUKURU na kuipa ushirikiano pale inapohitajika.

'KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU'

IMETOLEWA NA:

Sabas Salehe

NAIBU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA